

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI**

**22 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 22 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **386. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ambayo ujenzi wake umesimama.

#### **387. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaunga mkono jitihada za Wananchi wa Kilimanjaro kwa kumalizia ujenzi wa maboma ya Zahanati na Vituo vya Afya.

#### **388. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa kibali cha ajira za Watendaji wa Kata na Vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

**389. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati majengo ya Shule za Msingi chakavu Wilayani Masasi yaliyojengwa kati ya Mwaka 1905 na 1960.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**390. MHESHIMIWA AMINA DAUD HASSAN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa kutenga fedha ya mabadiliko ya Tabianchi kusaidia Wananchi wenye visima vya maji chumvi Zanzibar.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**391. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga *Campus* ya Chuo Kikuu Mzumbe katika Mkoa wa Singida.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**392. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kwa namna gani Serikali inatekeleza Kanuni ya Kimtandao ya *Network Neutrality* katika utoaji na upatikanaji wa huduma za jamii.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**393. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mikakati gani ya kudhibiti mifugo katika Bonde la Ihefu na Mto Kilombero.

**WIZARA YA MAJI:**

**394. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA  
(MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga Miradi ya Maji katika Vijiji vya Mateka, Tukuzi, Kitelea na Sepukila Wilayani Mbinga.

**395. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL  
ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Mji Mdogo Gairo watapata maji ya kutosha.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**396. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA  
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mangaka hadi Morogoro kupitia Mbuga ya Selous utaanza kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO  
WA AFRIKA MASHARIKI:**

**397. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR  
(BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Balozi za Tanzania zinatumia vipi fursa ya kukua kwa lugha ya Kiswahili Duniani kutafuta ajira kwa Watanzania.

**WIZARA YA KILIMO:**

**398. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS  
NDAKIDEMI (MOSHI VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itarejesha utoaji ruzuku ya pembejeo za dawa kwa Wakulima wa Kahawa ili wazalishe zaidi kama awali.

**WIZARA YA AFYA:**

**399. MHESHIMIWA BENARDETA KASABAGO  
MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga Hospitali kubwa katika Mkoa wa Kagera.

**WIZARA YA NISHATI:**

**400. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini mradi wa kuunganisha umeme wa *Grid* ya Taifa kutoka Nyakanazi hadi Kigoma utaanza.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
22 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**